

**AJAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Simu: +255 26 296 3311  
Nukushi: +255 26 296 3315  
Barua pepe: [acz@ardhi.go.tz](mailto:acz@ardhi.go.tz)  
Tovuti: [www.ardhi.go.tz](http://www.ardhi.go.tz)  
Unapojibu tafadhali taja:



Idara ya Maendeleo ya Makazi,  
Mkoa wa Dodoma,  
S. L. P. 1062,  
**DODOMA**

**Kumb. Na. LD/DOM/58218/10**

**30 Mei, 2023**

Mkurugenzi Mtendaji,  
Kituo cha Uwekezaji Tanzania,  
S. L. P. 938,  
**DAR ES SALAAM.**

**YAH: MAOMBI YA UTHIBITISHO WA UMILIKI WA KIWANJA NA.1 KITALU "AH"  
MJI MPYA- VEYULA KATIKA JIJI LA DODOMA**

Rejea kichwa cha habari hapo juu pamoja na barua yako yenye **Kumb. Na. CA.148/234/01D/135** ya tarehe 22 Mei 2023 kuhusiana na somo tajwa hapo juu.

2. Baada ya kufanya upembuzi tumebaini hakuna kumbukumbu za umiliki zilizosajiliwa katika Ofisi za Ardhi Mkoa wa Dodoma hata hivyo Ofisi yetu imepokea barua yenye **Kumb. Na. CCD/LD/172142** ya tarehe 13 Aprili 2023 **kutoka** kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuhusiana na maombi ya utengaji wa eneo husika kuwa eneo la uwekezaji .

3. Katika Barua hiyo Halmshauri ya Jiji wametujulisha kuwa licha ya eneo husika kutengwa na Mamlaka hiyo kama eneo la uwekezaji, bado lilikuwa chini ya umiliki wa asili wa Kampuni ya **Swaje Plan Limited** ambao waliingia mkataba wa mauziano ya Ardhi hiyo na Kampuni ya kigeni ya **Mainland Group Agro Process Tanzania CO. Limited.**

4. Pamoja na barua husika, Halmashauri ya Jiji wamewasilisha nakala ya mkataba wa mauziano ya ardhi husika baina ya **Swaje Plan Limited** na **Mainland Group Agro Process Tanzania CO. Limited.** Aidha, Ofisi ya Ardhi Mkoa inaendelea na hatua za uchakataji maombi husika kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu

5. Nashukuru kwa ushirikiano.

G.G. Mboha

**Kny:KAMISHINA WA ARDHI MSAIDIZI  
MKOA WA DODOMA**

**Nakala: -** Mkurugenzi wa Jiji,  
Halmashauri ya Jiji la Dodoma,  
S. L. P. 1249,  
**DODOMA.**

(Kwa taarifa)